HISTORIA NA UTAMADUNI WA TEMEKE

Joyce na Moshi

Manispaa ya Temeke ni moja ya Halmashauri chache kongwe zenye utajiri na historia ambayo imechangia kuleta mabadiliko kisiasa, kiuchumi na kijamii nchini. Kwa ujumla Temeke imekuwa kitovu cha upatikanaji wa uhuru wa Tanzania bara, pia kwa ukuaji wa michezo, utamaduni na maendeleo ya kilimo katika jiji la Dar es Salaam.

Temeke ni moja ya Wilaya inayolibeba Jiji la Dar-es-Salaam, kivipi, Dar-es-Salaam ni Temeke kwa kuwa bandari ipo Temeke,viwanja vyote vya mipira kitaifa - Uwanja wa Taifa na uwanja wa Uhuru, pia ipo jirani na Uwanja wa ndege wa kimataifa, ni mwanzo wa Reli ya Tazara, ina Uwanja wa kimataifa wa maonesho - sabasaba, ina daraja la Nyerere ambalo ni la kimataifa.

Samaki hupatikana kwa uwingi Temeke, ina fukwe nzuri za kuvutia zenye mchanga mweupe, ina wakazi wengi na wahamiaji wanaopata maeneo ya kujenga kutokana na kuwa na maeneo makubwa tena ya wazi.Ina mtandao mkubwa wa barabara za lami.hii ndiyoTemeke tunayoisema.

Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, idadi ya wakazi wake ni 1,368,881 kati ya hao wanawake 699,825 na wanaume 669,056.

Kijiografia Temeke ina ukubwa wa Kilomita za mraba 656 kabla ya kugawanywa na kuzaliwa Wilaya mpya ya Kigamboni,

Kwa upande wa Mashariki, Temeke imepakana na bahari ya Hindi, Kusini kuna Wilaya ya Mkuranga na Magharibi kusini kuna Wilaya ya Ilala kwa kufuata reli ya kati

Lakini wapo wanaojiuliza nini asili ya Temeke na watu wake?, Swali hilo linajibiwa vizuri na Mzee Abdallah Maloka ambaye ameishi eneo hilo kwa miaka mingi.

Mzee huyo ambaye anaonekana kuwa na nguvu, alisema katika kipindi cha nyuma Temeke ilikuwa eneo lenye mapori mengi na sehemu ambazo watu walikuwa wakiishi ni Chang'ombe, Keko- Magulumbasi, Mbagala kizuiani, Rangitatu na Tandika.Yeye alikuwa akiishi eneo lililokuwa likijulikana kama nyani na Ngedele kwa sasa panaitwa Unubini Kata ya Chang'ombe,wakati huo akiwa kijana mdogo baada ya kuajiriwa alihamia Kata ya 14.

Alisema maeneo ambayo kwa sasa kuna viwanja vya michezo ikiwamo Uwanja wa Taifa na ule wa Uhuru kulikuwa kiwanja cha ndege ndogo za jeshi. Eneo ilipo Salvation Army hivi sasa palikuwa na karakana ya ndege hizo, uwanja huo uliambaa kuelekea ilipo Equitor grill Mtoni kwa Aziz ally ndiko ndege ilikuwa ikipaa.

"Wengi tulikuja maeneo haya kwa ajili ya kuwinda wanyama wadogo wadogo na ndege, nakumbuka tulitembea porini kwa kufuata njia nyembamba ya wapita kwa miguu ambayo kwa sasa ni barabara ya Mandela kutafuta kitoweo," alisema Maloka.

Hata hivyo uwanja wa ndege ulihamishwa baada ya wakoloni kujenga uwanja wa Uhuru katika shamba la bibi ndivyo palivyokuwa pakijulikana hapo zamani na kambi ya jeshiya Twalipo kujiongeza zaidi.

Maloka alisema eneo ambalo kwa sasa kuna ofisi za Manispaa kulikuwa na mashamba ya mpunga kutokana na kuwa na maji maji yakutosha kilimo hicho.

Maloka anafichua kwamba eneo ambalo kwa sasa kuna soko la Tandika,lilikuwa ni shamba la mikorosho, baada ya kufyekwa tulitengeneza kiwanja ambacho ngoma za ya Tokomile ilikuwa ikichezwa hapo siku za mwisho wa wiki na Temeke stereo kulikuwa mashamba ya nguvu kazi kwa ajili ya vijana.

NINI ASILI YA TEMEKE?

Maloka alisema bado jina hilo limekuwa na utata, ingawa kuna baadhi ya maelezo yanayosema jina la Temeke lilipatikana wakati wa mvutano wa mashindano ya ngoma za makabila ya Wandegereko na Wazaramo. Alisema katika ushindani wa ngoma hizo za asili, jina la Temeke lilizaliwa na watu walianza kutumia kutambulisha eneo hilo.

“Nakumbuka wakati nikiwa mdogo hadi nina umri wa ujana kulikuwa na mashindano ya ngoma yakifanyika kila mwisho wa wiki, watu walicheza ngoma na wengi tulikuwa tukienda kuangalia mashindano hayo ya ngoma, walioshindwa waliambiwa wanatetemekea na ndipo likatoka jina la Temeke,” alisema.

Hata hivyo alieleza dhana ya chanzo cha jina hilo zipo nyingi, kila mmoja anasema kile anachokijua lakini ukweli utabaki kuwa Temeke ni jina kongwe katika jiji hili la Dar es Salaam.

KUSTAWI KWA TEMEKE

Ustawi na maendeleo ya Wilaya ya Temeke ulianza kuchanua tokea mwaka 1984 mara baada ya kujengwa jengo la ofisi ya Wilaya na kidogo kidogo taswira yake ilianza kubadilika.

“Nakumbuka jengo la kwanza kujengwa kama ofisi lilikuwa la mbao, pale penye uwanja wawazi wa Mkuu wa Wilaya ya Temeke. jengo hilo lilikuwa na vyumba vingi sana ikiwamo ofisi Mkuu wa Wilaya wakati ule alikuwa Mheshimiwa Bernadetha Kunambi, Mkurugenzi wa wa kwanza alikuwa Bwana Matembele na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) alikuwa Mzee Nasoro Msangi,” aliongeza kusema. muda huo mimi nilikuwa nimeajiriwa kama mtendaji.

Mwaka 1990 kulijengwa jengo la sasa la Mkuu wa Wilaya, na hivyo Mkuu wa Wilaya ,Mkurugenzi na watendaji wa Idara walihamia humo, Mkuu wa Wilaya alitumia ofisi za upande wa Mbele na Mkurugenzi na wakuu wa Idara walitumiwa Ofisi za nyuma ambazo ni ofisi za

Uhamiaji hivi sasa.

Mradi wa shirika lisilo la kiserikali DSSD ambao walijishughulisha na kuzuia malaria na maji machafu, walijenga vibanda vidogo vidogo na vyoo vingi ambavyo walitumia kufundishia wananchi, eneo ilipo Mahakama ya Wilaya ya Temeke hivi sasa. Lakini walipoondoka majengo hayo yalitumiwa na watendaji wa Serikali idara mbalimbali zikiwemo Elimu, Ardhi na Biashara.Maloka alisema

Kwa upande wa elimu, kulikuwa na Taasisi tatu za elimu tu, kulikuwa na shule ya sekondari ya Kibasila, Chuo cha ualimu Chang'ombe na Shule ya msingi ya Chang'ombe, ambayo ilikuwa ikichukua watoto wa wahindi na watendaji wa serikali tu, shule hivi sasa inajulikana kama shule ya mazoezi- Chang'ombe.

Maeneo ya Starehe yalikuwa ni ngoma za kienyeji Tandika lilipo soko hivi sasa, ngoma za Tokomile zilikuwa zikichezwa huko , na Mwembe Yanga kulikuwa na ngoma za Wamatumbi, kwa Sokota -Muundo bar siku za mwisho wa wiki Dar jazz walikuwa wakitumbuiza hapo, Kibondemaji kulikuwa na ngoma za wamakonde.

Keko Magulumbasi kihistoria, ilikuwa makazi ya Mzee Magulumbasi aliyekuwa mwanzilishi wa eneo hilo na inasemekana alitokea kusini mkoa wa Ruvuma, wengi wanaikumbuka vyema Magulumbasi kwa kuwa na pombe za kienyeji zilikuwa zinapikwa hapo na kunywewa , hata jina limebaki kuwa Magulumbasi.

Mtoni Kwa Aziz Ally hivi sasa ilikuwa ikijulikana kama Magogoni yalikuwa ni makao ya Frelimo, walikaa pia Mtongani kwenye nyumba za Kota pale ilipo shule ya msingi ya mama Mary na Marehemu Samora Machel alikuwa akifikia Kurasini pale kilipo chuo cha Diplomasia hivi sasa, Maloka aliongeza.

Kulikuwa na Mzungu mmoja kwa jina Bwana DOSA na familia yake sijui katoka nchi gani, alikuwa na nyumba yake pale Mtongani chini ya reli ya Tazara ambapo hivi sasa pamejengwa kwa muda Kanisa la EAGT la Askofu Katunzi, Mzungu huyo ameondoka miaka ya mwisho mwisho ya utawala wa awamu ya kwanza. sijui alikuwa akifanya nini ila amekaa muda mrefu sana, yeye na familia yake nakua nikimwona.

Mwaka 1996, Jengo la Elimu shule za msingi lilijengwa na Mkurugenzi akahamia humo.wakati huo alikuja Mkurugenzi marehemu Idd Nyundo yeye alikuwa Mkurugenzi wa Nne tangu mimi niajiriwe hapa.

Ilipofika mwaka 2000 baada ya kuvunjwa kwa Tume ya Jiji, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke chini ya Mkurugenzi Idd Nyundo,akiwa wa nne kuiongoza Temeke.

Mara baada ya kuundwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke mabadiriko kimaendeleo yalipaa kwa kasi sana na kuwa mfano wa kuigwa kati ya Halmashauri zote nchini.

Mwaka 2001, Mkurugenzi Nyundo alianzisha ujenzi wa jengo la utawala la ghorofa tatu ambalo liliwekwa jiwe la msingi na Mhe. Ally Mohamed Shein, na mwaka 2003 jengo hilo la utawala

lilifunguliwa na Mhe.Fredrick Sumaye aliyekuwa Waziri Mkuu wakati ule chini ya Meya, Mstahiki Abdallah Yakub**,** na Meya wa Jiji la Dar-es-salaam alikuwa Mstahiki Kitwana Kondo.

“Nyundo ndiye Mkurugenzi aliyefanya mabadiliko mengi ya Temeke, alikuwa mchapa kazi usiku na mchana hadi ile dhana kwamba Temeke ni mahali pasipofaa kuishi ilitoweka na kuwa kimbilio la watu wengi,”Alipima viwanja vya makazi Chamazi na Toangoma na kuwauzia watumishi kwa bei nafuu sana ili kila mtumishi apate kiwanja cha kujenga.Namkumbuka sana, alisema Maloka.

"Vile vile, asingekuwa yeye leo hii wengi tungekuwa nyuma, Nyundo ndiye aliyetufunua macho kwa siye tuliye achia elimu ya msingi; tulipewa nafasi ya kujiendeleza kusoma masomo ya jioni ili kupata cheti cha kidato cha nne, tulikuwa tunaruhusiwa kutoka mapema kwenda Wailes shule " alisema Maloka

Mkurugenzi Nyundo, alianzisha mpango wa kujenga barabara za lami ndani ya Manispaa ikiwamo Kichangani, Mahunda,na masoko, soko la Sterio, soko la Tazara, Tandika Kampochea na Mbagala Kampochea kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo ndogo. na jengo la ghorofa tatu la Utawala la hospitali yetu .

Nashukuru nimefanya kazi na awamu zote tano, na bado nina nguvu.Mzee Abdallah Maloka.

.